**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia afya njema na kuweza kukutana hapa leo hii, katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Baraza la Kumi la Wawakilishi ambao shughuli yake kuu ni kujadili Bajeti ya mwaka ya Serikali kama kifungu cha 88(b) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kinavyoeleza.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri wenye kuzingatia uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye malengo na unaozingatia matokeo chanya kwa manufaa ya wananchi anaowaongoza. Hii, inathibitisha kiu na utashi mkubwa alionao wa kuwaeletea maendeleo wananchi na kutekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kumpa afya njema, hekima na busara katika kuliongoza taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na muelekeo wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 ili kuhakikisha makusanyo ya fedha za Umma na Matumizi yake kupitia Wizara hii yanafanywa kwa kuzingatia misingi ya sheria na kanuni ziliopo.

**Mheshimiwa Spika,** Nitumie pia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri , Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa utendaji wao mzuri wa kazi zao na ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati hii katika kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Halkadhalika, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Wajumbe wa Kamati yangu kwa kazi nzuri wanayoifanya na ushirikiano wanaouonesha kwa pamoja katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu kwa muda wote, naomba sasa niwatambue Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Yahya Rashid Abdulla Mwenyekiti
2. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Foum Mussa Mjumbe
4. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Mjumbe
5. Mhe. Bahati Khamis Kombo Mjumbe
6. Mhe. Kombo Mwinyi Shekhe Mjumbe

Aidha, Kamati hii kazi zake zinaratibiwa na Makatibu wawili ambao wanatusaidia kutekeleza majukumu yetu kitaalamu na kiufanisi. Makatibu hao ni:-

1. Ndg. Rahma Kombo Mgeni - Katibu
2. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi iliendelea kutekeleza Programu zake tatu ambazo ni:-

1) Program ya Usafirishaji

2) Programu ya Teknolojia ya Habari

3) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na usafirishaji.

PROGRAM YA USAFIRISHAJI

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia Program Kuu ya ***Usafirishaji,*** Kamati inaipongeza Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabani kwa kuanzisha adhabu za papo kwa papo kwa wanaokiuka Sheria na Kanuni za usalama barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na pongezi hizo, Kamati yangu bado haijaridhishwa na matokeo ya utendaji wa utaratibu huo kwani wakati tunapitia Bajeti ya Wizara hii iliripotiwa kuwa kwa kipindi cha mwezi wa Machi hadi Aprili, 2023 jumla ya makosa **1,540** kati ya makosa **4,910** yalikuwa bado hayajalipiwa faini jambo ambalo kimtazamo halileti tija kwani **Tsh. 36,041,000** ikiwa ni mapato ya Serikali yalikosekana ingawa kanuni ya 7 ya Kanuni za Adhabu za Papo kwa Papo imetoa nafasi zaidi kwa watuhumiwa wa makosa hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, Kamati yangu inaiomba Mamlaka kuchukua jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa utaratibu huu ulioanzishwa unaleta tija ili kutimiza azma na shabaha zilizokusudiwa za kuanzisha mfumo huu. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuzitumia CCTV Kamera zilizowekwa ili kuwakamata wanaovunja kanuni hiyo, kufanya tathmini ya matumizi ya mashine zinazotumika kwa ajili ya kutoa stakabadhi za malipo ili kupima ni kwa kiasi gani mashine hizo zinatumiwa na Wahusika na kadhalika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaipongeza Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, kwa kujipanga vizuri katika kusimamia Shughuli za Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji ikiwemo kuweka wakusanyaji wa ada za shughuli hizo kwa gari ambazo hazina kibali au ruhusa ya kisheria ya kufanya hivyo, ikiwemo gari za mizigo kutoka nnje ya Zanzibar na kuisambaza katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Hata hivyo, Kamati yangu iliarifiwa kwamba Mamlaka inashindwa kukusanya ada hizo wakati wa usiku huko Bandarini.

**Mheshimiwa Spika,** Kitendo hicho kinaikosesha sana mapato Serikali kwani Mamlaka hii bado haijaanzisha utaratibu wa kuwapangia kazi Wafanyakazi wake hadi muda wa usiku kwa madai kuwa inakabiliwa na uhaba wa Wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati haikuridhika na sababu iliyotolewa na Mamlaka na kwa msingi huo, inaitaka Serikali kuwaruhusu Mamlaka kuajiri Wafanyakazi ili Mamlaka iweze kupanga vyema shughuli zake kwa lengo la kuongeza mapato ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu bado inashauku ya kuona matokeo mazuri na ya muda mrefu ya Programu ya Usafirishaji kwa kupatikana kwa miundombinu na huduma za usafirishaji zilizo bora, salama na endelevu, hata hivyo, viashiria vya matokeo vilivyowekwa bado tunadhani haviakisi matarajio hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imelazimika kutamka hivyo kwa kuwa katika shughuli za utunzaji na matengenezo ya barabara mpya na kongwe tumekuwa tukishuhudia mashimo mengi kila kona, ukosefu wa alama na michoro ya barabara, kutuwama kwa maji barabarani pamoja na kukatwa mara kwa mara barabara hizo muda mfupi tu baada ya kutengenezwa kwa ajili ya huduma nyengine za kijamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ilikutana na Watendaji wa Wakala wa Barabara katika mizunguko yote ya kazi za Kamati na kubaini kwamba shughuli nyingi za Wakala ikiwemo kujenga na kufanya matengenezo barabara mbali mbali za Unguja na Pemba, matengenezo ya misingi ya maji ya mvua na zege kwa barabara kuu, ujenzi wa madaraja na makalvati, uwekaji miundo mbinu ya usalama barabarani zinafanyika kwa kasi ndogo kutokana na ukosefu wa fedha kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inalithibitisha hili, kufuatia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambapo anaripiti kwamba, hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023 Wakala wa Barabara Zanzibar alipatiwa asilimia **68%** ya fedha kwa kazi za kawaida na mishahara na asilimia **12.6%** tu ya fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengeneo ya barabara mbali mbali za Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na asilimia hiyo ndogo iliyopatikana, Kamati yangu inajiuliza, ni kweli Serikali itaifikia shabaha ya matokeo mazuri, endelevu na yenye tija kutokana na uingizwaji huu wa fedha?

**Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu hizo nilizozieleza ni dhahiri kuwa bado kuna safari ndefu ya kufikiwa ya malengo ya Programu ya Usafirishaji kwa upande wa Usafiri wa barabarani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati yangu inashauri Serikali kuhakikisha kuwa inaingiza fedha zote zilizotengwa Taasisi hii kwa ajili ya kuanza na kukamilisha kwa wakati uliopangwa miradi ya uimarishaji Usafiri wa Barabara ikiwemo Barabara za Mjini (**Km 100.9),** Barabara za Ndani (**Km 275.9)** pamoja na Barabara Kuu Nne za Zanzibar **(Km 125.6).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa barabara zilizojengwa kwa teknolojia mpya ya lami baridi, Kamati yangu ilikagua mradi wa ***Barabara za Ndani (Km 275.9)*** kwa kutembelea barabara za Jumbi - Kibondeni, Jumbi - IPA, Tunguu - Ndijani, Dunga – Zuze.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara yake hiyo, Kamati yangu ilibaini kwamba barabara hizo licha ya kuwa zimekamilika, bado zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mitaro suala ambalo linapelekea kutuwama kwa maji mengi katika baadhi ya sehemu jambo linalopelekea barabara hizo kuanza kuharibika ndani ya kipindi kifupi tu.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu imepatwa na wasi wasi mkubwa juu ya uimara wa barabara hizo zilizojengwa kwa teknolojia mpya ya lami baridi, na hasa ikizingatiwa kuwa katika barabara hizo kumewekwa alama zinazozuia kupita kwa gari kubwa wakati baadhi ya maeneo yaliyowekwa barabara hizo bado ni miji mipya hivyo wananchi wanahitaji kuiendeleza miji hiyo kwa kujenga nyumba na kadhalika, Mheshimiwa Spika, mfano mzuri wa eneo kama hilo ni eneo la Jumbi - IPA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yangu inaunga mkono juhudi za Serikali ilizochukua katika kujenga barabara hizo, hata hivyo, Kamati hii inaishauri Serikali kufanya uchunguzi wa kina juu ya maeneo yanayotarajiwa kujengwa barabara zenye uasili kama huo ili barabara hizo ziweze kuduma kwa muda mrefu kama inavyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuimarisha usafiri wa anga, ikiwemo kuanza matayarisho ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba. Tunaamini hatua hii ya kuanzisha mradi huu wa kimkakati ni miongoni mwa miradi itakayosaidia katika kutimiza azma ya Rais wetu Dkt. Hussein Mwinyi ya kuifungua Pemba Kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imeridhishwa na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuimarisha miundombinu ya usafiri wa baharini ikiwemo ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani, Bandari za Malindi, Mkokotoni, Shumba, Mkoani na Wete.

**Mheshimiwa Spika,** Tunawaomba Wasimamizi na Wajenzi wa bandari hizo kuthamini juhudi za Serikali kwa kutekeleza shughuli hizo kwa wakati ili ziende sambamba na kasi ya Serikali ya Awamu ya Nane ya kuwaletea wananchi maendeleo ikiwemo kupatikana kwa miundombinu na huduma za usafirishaji zilizo bora, salama na endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la Usafiri wa majini kati ya Pemba - Unguja na Tanga bado ni changamoto inayowakwaza wananchi wetu na Serikali kwa ujumla, hivyo, Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuifanyia matengenezo Meli ya MV Mapinduzi II ili kupunguza changamoto ya usafiri katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilibahatika kukaguwa matengenezo hayo na kushuhudia kazi kubwa inayoendelea ya kusawazisha mitambo na mifumo yenye hitilafu. Mheshimiwa Spika, Kamati inawashauri Mafundi wetu wazalendo kuwa bega kwa bega na Wahandisi kutoka nchi ya Korea ambao wanaifanyia ukarabati meli hiyo ili wajifunze na kufahamu kwa vitendo mifumo ya meli hii ili siku za baadae waweze kutekeleza jukumu hilo wao wenyewe jambo litakalopunguza matumizi ya fedha nyingi za Serikali.

## PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

**Mheshimiwa Spika,** tukigusia Programu ya Tekolojia ya Habari na Mawasiliano, naomba moja kwa moja tufanye rejea ya **Kifungu PP0103** ambapo tunashuhudia ongezeko la makadirio ya bajeti ijayo ambayo ni takriban asilimia mia moja ukilinganisha na makadirio ya bajeti ya mwaka unaomalizika kwa ajili ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeko hilo kubwa lililobainika, Kamati yangu ilitaka kupatiwa ufafanuzi juu ya shughuli zilizopangwa hata kifungu hicho kikafikia kiwango husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na matakwa hayo ya Kamati, tulielezwa kuwa kiasi hicho cha fedha kimetengwa kikubwa ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kiutendaji kutoka Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA na kuwa Shirika la Mawasiliano pamoja na kuufanyia Mkonga matengenezo makubwa yanayotarajiwa kutokea kutokana na ujenzi wa barabara mbali mbali ikiwemo barabara ya Tunguu – Makunduchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na athari kubwa itakayojitokeza kutokana na ujenzi wa barabara mbali mbali Kamati yangu inaishauri Serikali kuandaa Tume Maalum itakayo washirikisha Wataalamu wa miundombinu ya Barabara, Mawasiliano, Maji na Umeme pamoja na Wataalamu wa Mipango Miji na Vijiji ili kukaa pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji wa Miradi kwa lengo la kuepusha uharibifu wa miradi hiyo ndani ya muda mfupi wa matumizi yake kitendo kinachopelekea kuitia hasara Serikali.

## PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara, tunashuhudia kushuka kwa makadirio ya mapato ya Afisi Kuu Pemba kutoka **Tsh. *891,474,000*** kwa mwaka wa bajeti unaomalizika hadi **Tsh. *20,000,000*** kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ilitaka kupatiwa maelezo juu ya upungufu huo na ilielezwa kuwa upungufu huo umetokana na vyanzo vingi vya mapato kutoka Afisi Kuu Pemba sasa kuhamishiwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama wa Bararani.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Afisi Kuu Pemba kuendelea kusimamia malipo ya fidia kwa miradi mbali mbali inayotekelezwa na Wizara huko Pemba pamoja na kulifanyia matengenezo jengo lake la Ofisi liliopo Chake Chake ili kuweka mazingira mazuri kwa Wafanyakazi wake.

HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia hotuba yangu, Kamati inaiomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha kuwa wanasimamia vyema ukusanyaji wa mapato kupitia vianzio vyao vilivyopo ili kuweza kuongeza ufanisi katika kazi zao pamoja na kuipatia mapato Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, tunaiomba Serikali kupitia Bajeti hii ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuiingizia fedha kwa wakati na kwa kiwango chote kilichoombwa Wizara hii ili kila Taasisi zilizomo chini yake ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kukamilisha malengo yao kwa maendeleo ya Wananchi na Nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu na pia ninawashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** Niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mhehimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha.

Ahsante,



………….………………..

**(Mhe. Yahya Rashid Abdulla)**

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**